

# Watoto wa nta

 Southern African Folktale

 Wiehan de Jager

 Mutugi Kamundi

 2

 Kiswahili 



Hapo zamani za kale, paliishi familia yenye  
furaha.



Hawakugombana hata kidogo. Watoto  
waliwasaidia wazazi nyumbani na shambani.



Lakini, walikatazwa kwenda karibu na moto.



Walifanya kazi zao zote usiku. Hii ni kwa  
sababu walikuwa wameumbwa kwa nta.



Lakini, kijana mmoja alitamani kwenda nje wakati wa mchana.



Siku moja tamaa ya kwenda nje ikazidi.  
Wenzake wakamwonya asiende juani. Lakini,  
hakusikia.



Aliyeyuka kwa sababu joto lilikuwa kali.



Watoto wa nta walihuzunika walipoona kaka  
yao akiyeyuka.



Wakapanga jambo fulani. Walichukua nta  
iliyoyeyuka wakatengeza ndege.



Wakamweka ndege huyo juu ya mlima mrefu.



Jua lilipochomoza asubuhi, akapeperuka  
akiimba kwa furaha.



# Global Storybooks

[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)

## Watoto wa nta

- ✍ Southern African Folktale
- ✉ Wiehan de Jager
- ☞ Mutugi Kamundi

